

# KITEGA UCHUMI


**MARC ELLISON**
SKRIPTI / PICHA / VIDEO

**CHRISTIAN MUGARURA**
MICHORO


NAJAWA NA UCHUNGU KILA NINAPO WAANGALIA...
KILA SIKU NG'OMBE HAWA HUNIKUMBUSHA KUWA WAZAZI WANGU WALINIUZA KWA MWANAUME ILI NIKAWE MKEWE
... NILIKUWA NA MIAKA 14 TU.


WALINITENDA KAMA MFUGO- BIDHAA YENYE KUNUNULIWA NA KUUZWA.
KULIKO KUPITIA HAYA YOTE WAKATI MWINGINE HUWA NATA-MANI NINGEZALIWA NG'OMBE.
NA CHA KUSIKITISHA ZAIDI, KATIKA KABILA LETU LA WASUKUMA HIYO IME-KUWA HATMA YA MABINTI KAMA MIMI...


KATIKA MKOA WA SHINYANGA NCHINI TANZANIA,PINDI BINTI ANAPOANZA KUOTA MATITI NA KUPATA HEDHI, ANATARAJIWA KUOLEWA.
SISI NI VITEGA UCHUMI AMBAO TUNAWEZA KUPUNGUZA UMASKINI WA FAMILIA ZETU.
JINA LANGU NI GRACE MASANJA NA HII NI HISTORIA YANGU...


BADO NINAMPENDA, LAKINI NIKIKUMBUKA YOTE YA NYUMA, HUWA NAMLAUMU SANA KAKA YANGU KWA YALIYONITOKEA.
NILIKUWA NAFANYA VIZURI DARASANI NA NILITAKA KUWA MUUGUZI WA HOSPITALI NITAKAPOKUWA MKUBWA.
LAKINI SIKU MOJA KAKA YANGU ALIJIUNGA NA KUNDI BAYA SHULENI...
ALIANZA KUNYWA POMBE, KUVUTA BANGI NA UTORO.
BABA YANGU ALIKUWA NA HASIRA SANA PINDI ALIPOGUNDUA...
SINTARUHUSU TENA YEYOTE KATI YENU KWENDA SHULENI- NI KUPOTEZA FEDHA ZANGU.
BABA YANGU HAKUJALI KUWA NILIKUWA NAONGOZA DARASA LANGU, NA KUWA NILITAKA KUBAKI SHULENI.
LAKINI SIKUMSIKILIZA BABA NA NILIENDELEA KWENDA SHULE.



LAKINI WAZAZI WANGU WALIFANYA MAISHA YANGU KUWA MAGUMU SANA.
NILIPORUDI NYUMBANI WALIHAKIKISHA HAKUNA CHAKULA CHOCHOOTE KILICHOBAKI KWA AJILI YANGU...
NILILALA NA NJAA MARA KWA MARA.
SIKU NYINGINE BABA ALINILAZIMISHA KWENDA NAYE SHAMBA KULIMA, HII ILINISABABISHIA KUKOSA MADARASA MENGI.
KWA KIPINDI HIKI NILI-KUWA NA MSONGO WA MAWAZO...
SIKUSHANGAA NILIPOFELI MITIHANI YANGU YA MWISHO WA MWAKA?
WAKATI WENZANGU WANARUDI SHULENI, BAADAYE YANGU ILI-KUWA IMEFUNGIWA SHAMBANI.


MIEZI MICHACHE BAADAE, MWANAUME ALIKUJA NYUMBANI KWETU NA KUOMBA KUONGEA NA BABA YANGU.
NILIPOKUWA NIKIRUDI KUTOKA KISIMANI MAMA YANGU ALINIITA KWENDA KUKUTANA NA MWANAUME HUYO.
NINAITWA SAMWEL
...NINAKUPENDA
NINATAKA KUKUOA.
ALINIELEZA HAYA INGAWA SIKUWAHI KUKUTANA NAYE KABLA.
NILIGUNDUA KUWA ALIKUWA AMEMPATIA BABA YANGU MAHARI YENYE THAMANI YA NG'OMBE KUMI NA MBILI KWA AJILI YANGU...
LAKINI MWALIMU WETU ALITUAMBIA KUWA SISI BADO NI WADOGO SANA KUOLEWA KISHERIA.
UNACHOFANYA NI KULA TU CHAKULA CHETU.UMEKWISHA ACHA SHULE – NINI KINGINE UTAFANYA?


NILIKATAA...NA MUME WANGU MTARAJIWA ALINIANGALIA WAKATI BABA YANGU ANANIPIGA KWA KUKOSA HESHIMA.
BABA YANGU HAKUELEWA KUWA NDOTO YANGU ILIKUWA NI KUPATA ELIMU KWANZA NDIO NIOLEWE.
KUZALIWA, NDOA NA KIFO NDIO MAFANIKIO MATATU YAONEKANAYO KATIKA MAISHA YA MTU - LAKINI MAFANIKIO YA KWELI HUJA KUTOKANA NA UCHAGUZI SAHIHI.


KILA SIKU BABA YANGU ALIPORUDI KUTOKA SHAMBANI, ALINIULIZA SWALI HILI...
UMEBADILISHA MAWAZO YAKO LEO?
KILA SIKU JIBU LANGU LILIKUWA LILELILE.
HAKUNA!
SIKU ILIKUWA NZURI KIDOGO PALE NILI-POPATA KIPIGO KWA DAKIKA TANO TU.
WHACK!!
ALIKUWA AKITUMIA MKANDA WA SU-RUALI, FIMBO, MATEKE NA NGUMI.
HATA NILIPOANGUKA CHINI, ALIENDELEA KUNIPIGA.


SIKU MOJA ASUBUHI, NIKIWA NDANI NAFAGIA, BABA YANGU ALINIITA NA KUNIAMBIA NITOKE NJE.
SAMWEL AMEKUJA KUCHUKUA ALI-CHOKILIPIA...
WAMEKUJA KUKUCHUKUA
HAYO YALIKUWA MANENO YA MWISHO BABA YANGU KUNIAMBIA.
TOFAUTI NA HAPO TUTAPOTEZA NG'OMBE ZOTE.


BABA YANGU NA SAMWEL WALISHAPANGA KILA KITU...
NA WAKATI ULE KULIKUWA HAKUNA WA KUNISIKIA WALA KUNISAIDIA, MAJIRANI ZETU WALIKUWA WAMEKWENDA SHAMBANI.
MAMA! MAMA!...


SAMWELI ALINIKALISHA KATIKATI YAKE NA RAFIKI YAKE ILI NISIWEZE KUTOROKA.
NILIANZA KULIA.
NIACHE, SITAKI KWENDA!


NILIJARIBU KUFURUKUTA, LAKINI MIKONO YANGU ILIKUWA IMEBANA KWA NGUVU NA SAMWELI.


NILIJARIBU KUONGEA NA MUME WANGU MPYA...
MIMI BADO MDOGO SANA KUOLEWA...
KAMA MKINIACHIA SITARIPOTI POLISI.
KATIKA MKOA WA SHINYANGA WA-NAUME WA KISU-KUMA WANA KAULI MBIU
ISEMAYO =
POMBE,
NYAMA NA
UKE...
WANAAMINI KWAMBA ILI KUWA MWANAUME WA KWELI NA MWENYE KUHESHIMIKA UNAHITAJI KUWA NA VITU HIVI VITATU.
HIVYO SAMWELI HAKUJALI MIMI KUWA MDOGO.
TULISAFIRI MASAA KADHAA NA NILICHOKUWA NIKIWAZA NI: KWANINI WAZAZI WANGU WA-NANIFANYIA HIVI?
NILIFIKIRI KUWA MAISHA YANGU YALIFIKA MWISHO...
NILIHISI KAMA HUU ULIKUWA MWISHO WA KILA KITU.


NILIKUWA SIFAHAMU CHOCHOTE-INAWEZEKANA HIYO ILIKUWA NI BARAKA...
HIVYO SIKUWA NAJUA NINI KITAKACHOFUATA.
HATUKUWAHI KUPATIWA ELIMU YEYOTE JUU YA KUJAMIIANA SHULENI.
SASA TULIA...
NILIJARIBU KUMZUIA LAKINI ALIANZA KUNIRUSHIA NGUMI NIKIWA NIMELALA CHINI YAKE.


NILIKUWA NALIA LAKINI HAKUACHA...
HIVYO NDIVYO NILIVYOPOTEZA BIKRA YANGU.
HIVYO NDIVYO MAISHA YALIVYOKUWA KWA MIEZI KUMI NA MOJA ILIYOFUATA. ILIKUWA NI BAHATI KWA SIKU KUPITA BILA KUTAKA TUFANYE MAPENZI.
ANGEWEZA KURUDI NYUMBANI AKIWA AMELEWA,
NA KAMA CHAKULA CHA USIKU HAKIKUWA TAYARI ANGENIPIGA...
KAMA NILIKUWA NIMELALA, ANGENIPIGA PIA...
KAMA SIKUFUNGUA MLANGO HARAKA ALIPOGONGA...
UNAELEWA KILICHOFUATA...


BAADA YA KUNIPIGA SANA, ALINIBAKA...
KUMBUKA, UKO MALI YANGU SASA...
MIMI KULIPWA BABA YAKO KADHAA NG'OMBE HIVYO SIWEZI KUFANYA KILE MIMI KAMA WEWE.
NILILALA MACHO USIKU KUCHA HUKU NIKISHANGAA KWANINI WAZAZI WANGU HAWAKUJA HATA KUNITEMBELEA.
TULIISHI MBALI SANA NA MJINI, SIKUFAHAMU HATA NJIA YA KUTOROKEA,WALA NAMNA AMBAYO NINGEWEZA KURIPOTI POLISI...
...INGAWA NILISHASIKIA HADITHI ZA POLISI WAPOKEA RUSHWA WANAOFUMBIA MACHO MAOVU YAFANYWAYO NA WANAUME.
NI KIFO CHA SAMWEL KILICHOTOKEA MIEZI KUMI NA MOJA BAADAYE AMBACHO KILIPELEKEA MWISHO WA MAISHA HAYA...
LICHA YA CHOCHOTE AMBACHO UNGEFIKIRI, HABARI ZA AJALI ALIYOIPATA YA PIKIPIKI HAZIKUNIFURAHISHA.
KWA WAKATI ULE NILIKUWA TAYARI NA MATHIAS.....MTOTO WETU WA KIUME.


DAKTARI ALINIAMBIA KUWA NILITOKWA NA DAMU NYINGI SANA KARIBU KUFA WAKATI NILIPOKUWA NIKIJIFUNGUA.
NILIKUWA MDOGO SANA NA MWILI WANGU HAUKUWA TAYARI KWA AJILI YA KUJIFUNGUA.
NI WAZI KWAMBA ASINGEKWEPEKA, NA NINAMPENDA SANA.
HIVI SASA MIMI NI MJANE NISIYE NA KIPATO, MWENYE ELIMU NDOGO, VIPI NITAWEZA KUMSAIDIA?
SIKUWEZA HATA KUMUDU KULIPA KODI, MUDA KIDOGO BAADA YA KIFO CHA SAMWELI NILIFUKUZWA,NILIFANIKIWA KUBEBA NGUO TU.
KWA SIKU NILIKUWA NIKITEMBELEA NYUMBA KWA NYUMBA KUOMBA MABAKI YA CHAKULA
...NA KUOMBA HELA YA NAULI NIWEZE KURUDI NYUMBANI.


USIKU TULILALA KWENYE NYUMBA AMBAZO HAZIJAMALIZIWA.
WAZAZI WANGU WALIKUWA NA FURAHA SANA NILIPOWASILI NYUMBANI.
WALIMUONA MATHIAS NA WALIDHANI KUWA NILIKUWA NIMEKWENDA TU KUWASALIMIA NA KUWAONYESHA MJUKUU WAO...
LAKINI NILIANZA KUWAELEZEA KILICHOKUWA KIMETOKEA.
BABA ALIBAINI KUWA SAMWEL ALIKUWA AMEKUFA NA KWAMBA SIKUWA NIMEKIMBIA...KINYUME NA HIVI MILA ZINAELEZA KUWA ANGETAKIWA KURUDISHA MAHARI.


LAKINI PIA NILIMWAMBIA KUHUSU VITU VYOTE MUME WANGU ALIVYOKUWA AKINIFANYIA KUANZIA SIKU NILIPOCHUKULIWA.


BABA ALISEMA MILA ZETU ZA KISUKUMA NI ZA KULAUMIWA- KWAMBA ANGENYANYASIKA KIJIJINI KAMA ASINGEMTAFUTIA MUME MTOTO WAKE WA KIKE.
BADA YA MUDA KUPITA BABA ALIKUJA KUKIRI KWAMBA ALIFANYA MAKOSA KUNILAZIMISHA KUINGIA KWENYE NDOA NA ALINIOMBA MSAMAHA...
TARATIBU TUNAKUWA BABA NA BINTIYE KWA MARA NYINGINE.


BABA ANANIAMBIA MAKOSA YAKE HAYAWEZI KUJIRUDIA,NA HIVYO MDOGO WANGU BIRHA MWENYE UMRI WA MIAKA MINNE ATAMALIZA ELIMU YAKE KAMA TU ATAKUWA NA HELA.
LAKINI KUSEMA UKWELI, NINAMHOFIA.
BAADA YA KUJENGA NYUMBA NYINGINE, ZIMEBAKI TU NG'OMBE SITA KATI YA ZILE KUMI NA MBILI.
HIVYO NINATAMANI SANA KUJUA KAMA BABA YANGU ATABADILI MAWAZO PALE MAISHA YATAKA-POKUWA MAGUMU.


LICHA YA KILA KILICHOKUWA KIMETOKEA, BABA ALIPINGA WAZO LA MIMI KUJIUNGA NA CHUO CHA UFUNDI STADI KUPITIA SHIRIKA LISILI LA KISERIKALI LIITWALO AGAPE.
HUSAIDIA WASICHANA KAMA MIMI KUJIFUNZA BIASHARA ILI WAWEZE KUJIKIMU KIMAISHA NA SIO KULAZIMISHWA KUOLEWA WAKIWA WADOGO.
BIRD-FLY


NI MATUMAINI KUWA NGUVU YA KIPATO HIKI CHA ZIADA KUTAPUNGUZA MAOMBI YA MAHARI KWA WAZAZI KAMA BABA YANGU.
WAKATI WENGI WETU WAMECHAGUA USHONAJI, RAFIKI YANGU NEEMA NI KUJIFUNZA JINSI YA KUWA WELDER.


HIVYO NILIMPINGA BABA NA KUONDOKA.
NIMESHAHITIMU SASA NA NIMEPANGA KUKODISHA CHEREHANI ILI NIWEZE KUANZA BIASHARA YANGU WENYEWE.
NA KUANZA MAISHA MAPYA KWANGU NA KWA MWANANGU MATHIAS.

# KUHUSU



MIEZI SITA JUU, GRACE BADO ANAISHI NA WAZAZI WAKE KATIKA NYUMBA ZAO SHINYANGA. KUMEKUWA HAKUNA SHINIKIZO ZAIDI KWA AJILI YAKE NA RE- KUOA. HAIWEZEKANI KUKUSANYA FEDHA YA KUANZISHA BIASHARA YAKE MWENYEWE AU KODI YAKE CHEREHANI MWENYEWE, GRACE SASA ANAFANYA KAZI SEHEMU YA MUDA KWA TAILOR NDANI. YEYE HUFANYA TU ZAIDI YA $1 KWA SIKU.



KITEGA UCHUMI ' NI COMIC TATU NA KUSHINDA TUZO- MPIGA PICHA MARC ELLISON. YEYE AMEFANYA KAZI BARANI AFRIKA TANGU MWAKA 2011. MARC AMEFANYA KAZI KWA MADUKA MENGI IKIWA NI PAMOJA NA 60 MINUTES, AL JAZEERA, BBC, DIE ZEIT, THE GLOBE AND MAIL, THE GUARDIAN, THE TORONTO STAR, NA VICE.KWANZA ONLINE GRAPHIC RIWAYA YAKE KUHUSU ASKARI WA KIKE MTOTO ALISHINDA WORLD PRESS PHOTO MULTIMEDIA TUZO MWEZI APRILI 2016. YAKE YA KWANZA COMIC 'GRAPHIC KUMBUKUMBU', KUHUSU ASKARI WA KIKE MTOTO, MSHINDI WA WORLD PRESS PHOTO MULTIMEDIA TUZO MWEZI APRILI 2016. KAZI YA MARC INAWEZA KUTAZAMWA KATIKA WWW.MARCELLISON.COM.



CHRISTIAN MUGARURA NI KUSHINDA TUZO- MSANII MSINGI KATIKA KAMPALA, UGANDA. KAZI ZAKE NI PAMOJA NA 'MVUA', 'JET', 'TEKKE 1 & 2', 'WATOTO WA VITA' NA 'GRAPHIC KUMBUKUMBU'. CHRISTIAN AMETUNGA KAZI KWA AL JAZEERA ENGLISH, DIE ZEIT NA THE TORONTO STAR. KAZI YA CHRISTIAN INAWEZA KUTAZAMWA KATIKA WWW.CHRISTIANMAFIGIRI.COM. CHRISTIAN ANAJITUMA COMIC HUU KWA MWANA WAKE MCHANGA ARI.